



**SHULE YASEKONDARI MAGUBIKE
S.L.P 1149- MOROGORO**

JINA LA MWANAFUNZI

S.L.P.....
.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAGUBIKE WILAYA YA KILOSA
MWAKA**

1. Ninafuraha kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha **KWANZA** katika shule hii mwaka **20.....**, **HONGERA NA KARIBU SANA**. Shule ya sekondari Magubike ipo umbali wa **km 2.5** kutoka kijiji cha Magubike. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **...../01/20.....** unatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo ukiwa na mzazi/mlezi wako, mwisho wa kuripoti ni tarehe **...../01/.....**, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wale watakaochelewa au kushindwa kuripoti shuleni ndani ya muda uliotolewa.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:

2.1. Sare ya shule:

• WAVULANA

- i. Suruali mbili (2) rangi ya damu ya mzee, yenye malinda mawili na upana wa chini ni inchi 17 au sm 43 na iwe na mkunjo.
- ii. Shati nyeupe mbili (2) za mikono mifupi aina ya TOMATO.
- iii. Tai yenye rangi ya suruali.
- iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu visivyo na visigino virefu.
- v. Soksi zenye rangi nyeusi jozi mbili (2) zisizo na urembo wowote.
- vi. Sweta rangi ya damu ya mzee.
- vii. Fulana zenye rangi ya blue iliyo kolea mbili (2)
- viii. Sare ya michezo ni bukta na fulana nyekundu.

• WASICHANA

- i. Sketi mbili (2) rangi ya damu ya mzee, mshono wa Linda box, urefu kutoka magotini ni inchi 9 au sm 23
 - ii. Shati nyeupe mbili (2) za mikono mifupi.
 - iii. Tai yenye rangi ya sketi
 - iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu visivyo na visigino virefu (bajaji haziruhusiwi)
 - v. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (2) zisizo na urembo wowote
 - vi. Sweta rangi ya damu ya mzee..
 - vii. Fulana zenye rangi ya blue iliyo kolea mbili (2)
 - viii. Wanaovaa hijab ifanane na shati la shule isiyo na urembo wowote na iwe ndefu
- MUHIMU:** Kitambaa cha sampuli kwa suluali na sketi kimeambatanishwa, kama kuna tatizo kwenye swala la sare ya shule, fika shuleni kupata ufafanuzi zaidi.

2.2. Vifaa vya darasani:

- i. English – Kiswahili dictionary (1)
- ii. Mkebe wa hesabu mmoja (1) (Mathematical set) **HII NI YA LAZIMA MWANAFUNZI ANAPORIPOTI**
- iii. Mkoba wa kubebea madaftari (Sio mfuko wa Rambo)
- iv. Madaftari kumi (10) makubwa (Counter book, Quire 2)
- v. Kalamu ya wino, kalamu ya risasi na rula ndefu sm 30

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji wa Elimu Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote na wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima, ikiwa ni pamoja na kufanya mitihani na majaribio mbali mbali (ni kosa kutofanya mitihani au majaribio)
- (c) Kujisomea kwa umakini wakati ukiwa nyumbani ni jambo la lazima ili kufaulu mitihani.
- (d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule ni jambo la lazima.
- (g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote unaotakiwa
- (i) Kutunza mali za umma (ukihalibu mali ya umma kwa uzembe/makusudi utalipia)

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUKUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji.
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kuievywa kama vile bangi, kokeini, mirungi, kubeli, n.k
- (e) Kupiga au kupigana.
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- (g) Kudharau alama za taifa (kama vile, wimbo wa taifa, bendera ya taifa, n.k)
- (h) Kuo au kuolewa.
- (i) Kupata au kusababisha mimba
- (j) kutoa mimba.
- (k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki mgomo na kuvuruga amani na usalama wa shule au watu wengine.
- (l) Kukataa adhabu halali kwa makusudi.
- (m) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

- (a) Medical Examination Form; ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya Serikali.
Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.
- (b) Kuchangia chakula cha mchana shuleni, kulingana na makubaliano ya kikao cha Bodi ya shule na Wazazi, Swala la chakula kwa mwanafunzi ni la lazima
- (c) Vifa vya usafi shuleni ni; Wasichana: ndoo kubwa ya plastiki, kwanja na mfagio wa chelewa.
Wavulana: jembe lenye mpini na mfagio wa chelewa.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MAGUBIKE

Mampejwa